Aina ya maombi Mungu anayosema kwayo katika muktadha huu siyo tu maombi ya Mfalisayo ambaye anasimama kwa ujasiri katika kanisa akiangalia chini juu ya wenye dhambi uko nje. Ni namna gani ni rahisi kwetu kuomba kama hivi. Tunaweza kuhisi vizuri na safi katika kingo za makanisa yetu, kuwa vipofu kwa hatia zetu wenyewe. Siyo maombi ya mmoja ambaye analaumu hali ya ulimwengu juu ya watu wengine, bali kwa yeye mwenyewe ambaye anamuomba Mungu awasamehe unafiki na kushindwa kwa moyo wake mwenyewe kuwa mfano anaohitajika kuwa. Maombi Mungu anayoitia kwayo ni maombi ya mtoza ushuru ambaye, amejinyenyekeza yeye mwenyewe, ametambua hatia yake na kuja kusafishwa na Mungu wake.

Maombi Mungu anayoyahitaji ni maombi ya kutubu. Ni maombi ya waamini wanaofahamu kwamba kukosekena kwa baraka ni, sehemu, ya matokeo ya dhambi zao wenyewe. Ni maombi ya mkristo ambaye amekuja kufahamu kwamba amemuangusha Mungu na hakutembea kikamilifu katika njia yake. Hakutumia kipawa chake kuleta mibaraka Mungu anayotamani katika ulimwengu kumzunguka yeye. Si kila mara amekuwa mfano wa kristo na mwangaza katika giza. Amepoteza rasilimali zake na kuzika kipawa chake, ameonyesha matunda kidogo kwa bwana aliyewekeza katika maisha yake.

Maombi Mungu anayoyahitaji ni kulilia msaada. Si maombi ya kujisifu ya mtu mmoja anayeamini anachokila kitu chini ya utawala. Hata hivyo ni sala ya Ezra ambaye alitambua kwamba bila ya uongozi wa Mungu na msaada

asingeliweza kukamilisha kusudi la Mungu. Haya ni maombi ya mmoja ambaye ametambua mahitaji yake. Ni maombi ya kuongozwa, hekima na nguvu.

Hatimaye, maombi haya pia ni maombi ya huruma na rehema. Hili ni ombi la ujasiri kutoka kwa mtu aliyemuangusha bwana wake, lakini ni kilio cha moyo wake. Mtu mnyenyekevu anafahamu kwamba Mungu anahaki ya kuondoa baraka hizi, katika sehemu, kwa sababu ya dhambi zake mwenyewe, Pia anatambua, vyovyote, kwamba Mungu ni Mungu wa rehema na huruma ambaye husamehe dhambi na kurejesha baraka zake kwa wale waliotubu na kurudi kwake. Hiki ni kilio cha mtu mwenye moyo wa unyenyekevu. Anatamani kuwa chombo cha baraka za Mungu na uponya tena. Kwa hili kuchukua nafasi ni lazima arejeshe ushirika na Mungu wake. Husihi kwa Mungu kurejesha ambacho dhambi zake ilimekiharibu.

Katika kifungu hiki, lengo linabaki kwa waamini. Ni muamini ambaye anatakiwa kunyenyekea na kuomba yeye mwenyewe. Hili linahitaji utambuzi wa hatia na uhitaji. Ikiwa tutapata upya na urejesho wa baraka, ni lazima iwe katika muktadha huu wa kukubali hatia, kukiri dhambi na kunyenyekea tukisihi rehema na huruma kurejeshwa tena kama watumwa waaminifu na wazaao matunda kwa bwana.

Cha kuzingatia:

Tunajifunza nini kuhusu unyenyekevu katika sura hii? Wewe ni mtu mnyenyekevu?

Kuna muunganiko gani kati unyenyekevu na maombi katika kifungu hiki?

Ni maombi ya namna gani ya Mfarisayo katika Luka 18:10-14 tofauti kutoka maombi ya mtoza ushuru? Umewahi kuwa na hatia ya kuomba maombi ya Mfarisayo?

Ni namna gani maombi yako na aina ya maisha yako yanaakisi kwamba unaamini katika uweza na uongozi wa Mungu?

Tunajifunza nini katika sura hii kuhusu huruma ya Mungu kuwaelekea wale ambao wanajinyenyekeza wao wenyewe na kuja kwake?

Kwa maombi:

Muombe Bwana akusaidie wewe kuona hatia yako na kumhitaji yeye katika njia kubwa. Muombe yeye akusamehe kwa upofu wako kwenye uhitaji wako mwenyewe.

Chukua muda kukiri kushindwa na dhambi zako kwa Mungu. Muombe akusamehe na kukurejesha katika ushirika wa ndani na yeye.

Muombe Mungu akuonyeshe namna anvyohitaji kukutumia wewe. Muombe yeye kwa imani zaidi na ujasiri katika kusudi lake kwenye maisha yako.

5

# KUUTAFUTA USO WA MUNGU

*Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu… kunitafuta uso na kuacha njia zao mbaya. (2 Nyakati 7:14)*

Tunawatofutisha namna gani watu kati ya mtu mmoja na mwingine? Kila mtu anasura ya kipekee. Hii inatutenga mbali kutoka kwa watu wengine wote. Tunawafahamu watu kwa sura zao. Sura ni muhimu zaidi kuliko maana ya kumtambua mtu, vyovyote. Pia inawakilisha sifa ya mtu binafsi. Wakati tukiona sura ya mpendwa mmoja, tunafikri mara kwa kile huyo mtu alivyo na maana kwetu. Ikiwa tumeona sura ya adui, tunakumbuka namna gani wametuumiza sisi. Ikiwa tumekuwa tunaona sura ya mtu fulani katika mamlaka, tunatambua nafasi yake na kuitikia sawasawa.

Tumeiona dhana hii katika Kutoka 33. Wakati Musa anamuuliza Mungu kumuonesha utukufu wake, Mungu alimwambia kwamba hakuna mtu angeliona uso wake ana kwa ana. Nukuu uhusiano kati ya sura ya Mungu na sifa ya utukufu.

*(18)Akasema nakusihi unionyeshe uso wako.(19) Akasema nitapitisha wema wangu wote mbele yako nami nitalitangaza jina la BWANA mbele yako nami*

*nitamfadhili yeye nitakayemfadhili nitamrehemu yeye nitakaye mrehemu. (20) Kisha akasema huwezi kuniona uso wangu maana mwanadamu hataniona akaishi. (Kutoka 33:18-20)*

Wakati Mungu anamwambia Musa kwamba hakuna mmoja angeliona uso wake na akaishi, alikuwa anamwambia kitu kuhusu sifa yake. Alikuwa anamwambia Musa kwamba uso wake unahusiana na utukufu wa Mungu. Enzi yake ilikuwa ni zaidi kuliko macho yetu yangeliweza kubeba. Utakatifu wake ungelituharibu sisi kama viumbe wenye dhambi. Kuutafuta uso wa Mungu siyo kitu cha kuchukua kiwepesi.

Yakobo alielewa hili wakati Mungu anaongea naye katika Mwanzo 32:30. Alipata mshituko kwamba alikuwa bado anaishi kusimulia kisa:

*Yakobo akaipaita mahali pale, Penueli, maana alisema" nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka."*

Mtume Yohana anatuambia kwamba mwitikio gani wa watu katika dunia utakuwa wakati Bwana akirudi katika dunia hii:

*(15) Na wafalme wa dunia na wakuu na majemedari na matajiri na wenye nguvu na kila mtumwa na mwungwana wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima. (16) Wakiiambia milima na miamba" tuangukieni tusitirini mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na hasira ya mwanakondoo!. (17) Kwa maana siku iliyokuu ya hasira yao imekuja naye ni nani awezaye kusimama." (Ufunuo 6:15-17)*

Nukuu hasa kwamba kilio cha wasioamini kwa miamba kuwaficha wao kutoka" uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi." Kuutafuta uso wa Bwana ni jambo zito sana. Mungu ni Mungu mtakatifu. Atahukumu dhambi na

kuwafichua wanafiki. Ikiwa unamuomba yeye kuangaza mwanga wa uso wake kwako au kanisa lako kuwa vizuri kuwa tayari kwa kile mwanga wa utakatifu utafichua. Watu wengi wakubwa wanaume na wanawake wa Mungu wameanguka mbele yetu wamevunjika mbele za mwanga wa uso wake. Dhambi ilifichuliwa hakujua kuwepo. Mtazamo uliibuliwa walihisi wamekuwa wafu kwa muda. Kusimama katika mwanga wa uso wake, tunaona sisi wenyewe kwa uhalisia sisi ni kina nani na tulipata aibu na kunyenyekea. Acha tuchukue muda sasa kuzingatia kile maandiko yanatufundisha kuhusu uso wa Mungu.

## KUUTAFUTA USO WA MUNGU INAHITAJI KURUDI KUTOKA DHAMBINI

Moja ya mafundisho wazi ya maandiko kwa kuzingatia uso wa Mungu ni kwamba Mungu huficha uso wake kutoka kwa wale wanaoendelea katika dhambi. Sikiliza kile Bwana alisema katika Mambo ya walawi 17:10:

*Kisha mtu awaye yote wa nyumba ya Israeli au miongoni mwa wageni wanaokaa kati yao atakayekula damu ya aina yoyote nitakunja uso wangu juu ya mtu huyo alaye damu nami nitamkatilia mbali na watu wake.*

Ilikuwa ni dhambi Kwa Israeli kula damu ya mnyama hilo ilikuwa ni uuaji. Mungu aliazimia kwamba angeliuficha uso wake dhidi ya mtu yoyote wanaonajisi miili yao kwa njia hii.

Nabii Mika alielezea sawa wakati anaandika katika Mika 3:4:

*Ndipo watakapomwomba BWANA asiwaitikie naama atawaficha uso wake wakati huo kwa kadri walivyotenda mabaya kwa matendo yao.*

Nukuu sababu ya Mungu kuuficha uso wake. Ni kwa sababu ya uovu wa watu wake waliyonia.

Anaongea na watu wake katika Kumbukumbu 32:20 Mungu anasema:

*“Akasema nitawaficha uso wangu” nitaona “mwisho wao utakuwaje maana ni kizazi cha ukaidi mwingi.”*

Ukaidi na kutokuwa waaminifu wa watoto wa Mungu inamsababisha yeye kuuficha uso wake kutoka kwa Israeli. Dhambi na uovu hututenga sisi na Mungu sababu ni mtakatifu. Ikiwa tunataka kuutafuta uso wa Mungu, tunatakiwa kwanza kushughulika na dhambi. Bwana aliwaambia watu wake katika Hosea 5:15 kwamba angeliuondoa uwepo wake hadi wakili hatia yao na kuutaka uso wake.

Nitakwenda zangu niparudie mahali pangu hata watakapoungama makosa yao na kunitafuta uso wangu katika taabu yao watanitafuta kwa bidii.

Nukuu muunganiko kati ya kukiri hatia na kuutafuta uso wa Mungu. Hatutegemei uso wa Mungu kung’aa juu yetu hadi kizuizi cha dhambi kiwe kimeondolewa.

Katika historia yote ya kanisa, mwanamke na mwanaume wa imani walimtaka Bwana katika njia tofauti. Waliutafuta uso wa Bwana kupitia kuabudu, maombi, huduma na sadaka. Vitu hivi ni muhimu lakini hakuna kimoja wapo hatimaye, kinaweza kuonyesha uso wa Mungu kwetu isipokuwa tumeshughulika kwanza na dhambi. Yesu alimwambia mtu aliyeleta matoleo hekaluni katika Mthayo 5:23 kwanza aende akapatane na ndugu yake. Asingeliweza kuutafuta uso wa Mungu katika kuabudu hadi ashughulike na dhambi yake kwa ndugu yake. Mungu anamwambia mme ambaye hamtendei mema mke wake kwa heshima katika Petro 3:7 kwamba angelizuia maombi yake kwa namna alivyomtendea mke wake. Wakati wale

ambao wanatumika kwa nguvu kupitia unabii, ishara na maajabu walimkaribia Bwana Mathayo 7:22-23, aliwaambia kwamba hawafahamu wao. Walikuwa hawajashughulika na dhambi zao. Kwa Sauli, ambaye ametoa sadaka yake ya kondoo juu ya madhabahu, Bwana alisema:" utii ni bora kuliko dhabihu"(1Samweli 15:22). Sauli asingeliupata uso wa Mungu katika sadaka yake sababu alifanya dhambi katika maisha yake. Ikiwa tunaenda kuutafuta uso wa Bwana, ni lazima kwanza tushughulike na dhambi.

Ikiwa unapitia ukame katika maisha yako ya kiroho au ikiwa inaonekana kwamba uso wa Bwana umefichwa kutoka kanisa lako, kisha kitu cha kwanza unachohitaji kufanya ni kuzingatia kile ambacho kinaweka uso wake kuacha kuangaza kwako. Sehemu ya kutazama ni katika moyo wako.

KUUTAFUTA USO WAKE INAMAANISHA KUWA NA HAMU YA UWEPO WAKE NA BARAKA.

Ni wazi kabisa katika maandiko kwamba wakati Mungu anaficha uso kuna ushahidi wa hili katikati yetu. Nukuu kile Bwana anasema katika kumbukumbu 31:17-18:

*Ndipo hasira yangu itakapokuwa juu yao siku hiyo nami nitawaacha nitawaficha uso wangu nao wataliwa tena watawajiliwa na mambo maovu mengi na mashaka hata waseme siku hiyo je kujiliwa kwetu na maovu haya si kwa Mungu wetu hayumo kati yetu? 18 Nami nitawaficha uso wangu kwa kweli siku hiyo kwa maovu yote waliyoyafanya kwa kuigeukia hiyo miungu mingine.*

Anaongea katika Yeremia 33:5 Bwana anasema:

*Lakini ni kuzijaza kwa mizoga ya watu niliowauwa katika hasira yangu na ghadhabu yangu ambao kwa ajili ya uovu wao wote nimeuficha mji huu uso wangu.*

Wakati Mungu akiugeuza uso wake kutoka kwetu, tunaliona hilo katika kanisa na nchi yetu. Nchi huomboleza. Dhambi na uovu umejaa. Katika makanisa yetu, ugomvi na ukosefu wa baraka ni ushahidi. Tunda la roho mtakatifu huonekana kuwa limekosekana. Kuutafuta uso wa Mungu ni kulilia kwa upya hizo baraka. Ni kutambulisha hali zetu bila Mungu. Ni kuona jinsi tulivyo wapotevu na wasio na tumaini bila maisha yake kupita kupitia sisi. Wale ambao wanautafuta uso wake, muda mrefu kwa uwepo wake kuwa umedhihirika. Hawakuwa radhi kuishi bila kuwa na ushahidi uliowazi wa baraka zake. Kama Musa alipiga kelele:" Kama uwepo wako hautaenda pamoja nasi, usitupeleke sisi kutoka hapa" (Kutoka 33:15). Hawakuweza kubeba mawazo ya kuishi bila kuwa na baraka za Mungu katika maisha yao na huduma. Hawakuweza kufikri maisha bila kuwa na uwepo wake. Walikuwa na mtazamo wa mtunga zaburi katika Zaburi 42:1-3 wakati anaandika:

*Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji vivyo hivyo nafsi yangu inaonekana shauku, ee Mungu. (2) Nafsi yangu inamwonea kiu Mungu, Mungu aliye hai lini nitakapokuja nionekane mbele za Mungu. (3) Machozi yangu yamekuwa chakula changu mchana na usiku pindi wanaponiambia mchana kutwa," yuko wapi Mungu wako."*

Sikiliza kwa kile Bwana alikuwa anasema kwa kanisa la Leudekia katika Ufunuo 3:20:

*Tazama nasimama malangoni nabisha mtu akiisikia sauti yangu na kuufungua mlango nitaingia kwake nami nitakula pamoja naye na yeye pamoja nami.*

Uwepo wa Bwana hakuwa na kanisa la Laudekia. Hawakuutafuta uso wa Mungu. Kwa kweli, hawakuonekana hata kutambua kwamba hakuwa katikati yao. Bwana, ambaye angelikuwa na kiini cha tahadhari

yao, alikuwa akibisha kwenye mlango akiwa na hamu ya kuingia ndani. Mara ngapi hili limekuwa likitokea kwenye makanisa yetu na maisha yetu leo kama waamini? Tumekuwa tukilenga sana juu ya shughuli zetu kwamba tunashindwa kuona kwamba Bwana hayupo. Kuutafuta uso wa Bwana ni kumualika yeye katika makanisa yetu na katika maisha yetu ya kila siku. Je! inakushangaza wewe kuwa nimesema hili? Siyo kusudi la Mungu kila mara kuwa katikati yetu? Maandiko yanatufundisha hapa kwamba hii siyo kila mara ni sababu. Wakati bado hajatuacha sisi, kila mara huacha mikutano na sherehe zetu. Kwa wakati uwepo wake huondolewa nje ya makanisa yetu. Kila mara hupuuzwa na njia zake hubezwa. Makanisa yetu na nchi yetu huteseka sana kama matokeo.

Habari njema ni kwamba Mungu yupo tayari kurejesha uwepo wake ikiwa tukirudi kwake na kuutafuta uso wake. Sikiliza katika ahadi yake katika Ezekieli 39:29:

*Wala sitauficha uso wangu tena kwa maana nimemwaga roho yangu juu ya nyumba ya Israeli asema Bwana MUNGU.*

Ni siku gani hiyo ya utukufu ingelikuwa. Mungu asingeliuficha uso wake kwa watu wake kwa muda mrefu. Siku ingelikuja ambayo angelimimina roho wake juu ya taifa la Israeli na wangeliufahamu tena uwepo wake wa kishangaza na baraka zake. Ni furaha yake kumimina kuburudiko na kufanywa upya kwa watoto wake. Ni matamanio yake kufanya uwepo wake kufahamika kwa wote ambao wanautafuta uso wake. Hili ni tamanio letu leo? Je tunahuzunika sababu uwepo wake haupo katikati yetu? Je tunapiga kelele kama Musa:” Ikiwa uwepo wako hautaenda nasi, usitupeleke kutoka hapa”(Kutoka 33:15)?

Wakati mwingine, ikiwa tuwaaminifu kwetu wenyewe, tu radhi na mambo jinsi yalivyo. Tunapenda kuwa katika

kudhibiti maisha yetu wenyewe. Hatutaki kitu chochote kubadilika. Yesu anagonga mlango, lakini hatupo tayari kuufungua kumuacha yeye aingie. Wakati anakuja katika hekalu katika Yohana 2:13-14, Yesu alitengeneza mjeredi na kuwatoa nje wavunja fedha na wauza wanyama. Wakati unautafuta uso, uwepo wa Mungu na baraka zake, usichangazwe ikiwa ametoa nje vitu vichache kutoka kati yenu. Labda kuna watu wameacha kanisa lako. Labda dhambi imedhihirishwa katika maisha yako. Anaweza kubadilisha muelekeo wa kanisa lako na kuwaweka watu wasiwe huru. Wakati unautafuta uso wa Bwana na kuualika uwepo na baraka zake, ni lazima ujiandae kumuacha yeye achukue udhibiti.

## KUUTAFUTA USO WA MUNGU NI KUTAFUTA MSAADA WAKE NA ULINZI

Katika Zaburi 69:17-18 mtunga zaburi anafanya uhusiano kati ya Mungu kuficha uso wake na uhitaji wa kuokoa kutoka kwa adui yake.

*(17) Wala usinifiche uso wako mimi mtumishi wako maana mimi nimo taabuni unijibu upesi. (18)Uikaribie nafsi uikomboe kwa sababu ya adui zangu unifidie.*

Mtunga zaburi anagundua kwamba maadamu Mungu anaficha uso wake, angelikuwa kwenye mahangaiko makubwa. Adui zake wangelimshinda yeye ikiwa Mungu asingelikuwepo kumsaidia. Alimhitaji Mungu aonyeshe uso wake na kumpa yeye msaada na uhitaji aliouhitaji.

Baadaye mtungaji wa zaburi anaandika:

*Eee BWANA unijibu hima roho yangu imelegea usinifiche uso wako nisifanane na washukao shimoni. (8) Unifanye kusikia fadhili zako asubuhi kwa maana nimekutumaini wewe. Unijulishe njia nitakayoiendea kwa maana nakuinulia nafsi yangu. (143:7-8)*

Nukuu kwamba mtunga zaburi aling'ang'ania kwa Mungu asiufiche uso wake kwake. Badala yake, aliomba udhibitisho wa pendo lake na kuongozwa katika njia apaswayo kwenda.

Kwa mtunga zaburi, kuutafuta uso wa Mungu alisema ni utambuzi wa udhaifu na kukosa uwezo kwake mwenyewe. Alikiri uhitaji wake wa nguvu na hekima. Anamuomba Mungu kumletea neno la upendo wake usioshindwa. Mtunga zaburi anakuja kwa Mungu kama mtoto mdogo anayetambua kwamba ikiwa Mungu hatakuja kwa msaada kwake, hakika angelipotea, ni kitu cha kuogofya kumuomba Mungu adhihirishe uso wake, lakini mtunga zaburi alifahamu kwamba hili lilikuwa ni tumaini lake la pekee. Alifika mwisho wa yeye mwenyewe. Hakuwa na ujasiri zaidi katika mwili na hekima yake mwenyewe. Aling'ang'ana na Mungu amuonyeshe njia ya kwenda na kuhaidi yeye mwenyewe kuifuata hiyo njia. Kulikuwa hakuna mfariji mwingine, hakuna hekima nyingine, hakuna nguvu nyingine ambayo ingemtosheleza. Mungu peke yake alikuwa jibu. Hakuna kitu kingine angefanya.

Hauwezi kuutafuta uso wa Mungu ikiwa unatafuta mambo mengine kwa wakati mmoja. Ikiwa unatafuta uso wa Mungu kwa hekima, unahitaji kurudi kutoka katika njia yako mwenyewe ya kufikri. Ikiwa unatafuta uso wa Mungu kwa nguvu, unahitaji kusitisha kuamini katika mwili wako. Vitu hivi vyote vinashindana tu na Mungu katika maisha yetu. Kuutafuta uso wa Mungu ni kutambua uhitaji wetu na kujitoa sisi wenyewe kusikiliza na kumfuata yeye mwenyewe.

## KUUTAFUTA USO WA MUNGU NI KUTEMBEA KATIKA UTII.

Hii inatuleta sisi katika kitu moja cha kuhitimisha kwa kusema kuhusu kuutafuta uso wa Bwana. Kuutafuta uso

wa Mungu ni kutembea katika utii. Mtunga zaburi alilipata hili wakati akisema katika Zaburi 119:57-59 :

*Bwana ndiye aliye fungu langu nimesema kwamba nitayatii maneno yake. (58) Nimekuomba radhi kwa moyo wangu wote unifadhili sawasawa na ahadi yako (59) Nalizitafakari njia zangu na miguu yangu nalizielekezea shuhuda zako.*

Mtunga zaburi anatuambia kwamba aliomba radhi uso wa Bwana. Kile cha muhimu kunukuu hapa ni namna ya kauli hii kuhusu kuutafuta uso wa Mungu ipo katika vifungu viwili imbavyo vinazungumza kutembea katika utii. Katika kifungu cha 57 mtunga zaburi anahaidi kutii maneno ya Mungu. Katika kifungu 59 anasema kwamba anazitafakari njia zake na kuelekeza hatua zake kwenye shuhuda za Mungu. Kwa mtunga zaburi, kuutafuta uso wa Mungu kuonyesha utii kwa neno lake.

Kuutafuta uso wa Bwana inahusisha kujitoa. Hakuna mmoja anaweza kuutafuta uso wa Mungu bila kuwa na ahadi hii. Kuutafuta uso wa Bwana ni kujitoa sisi wenyewe kutembea katika utii. Hii inahitaji" kuzitafakari njia zetu" na" kuzirejesha hatua zetu"(Zaburi 119:59). Wakati Mungu anaonyesha uwepo wake huja kubadilisha maisha yetu. Huja kuondoa vikwazo katika ushirika na baraka. Haikuwa kipimo cha muda mfupi kwa muda wa mgogoro. Hutubadili sisi milele na inahitaji muda mrefu wa ahadi ya maisha kufanya ushirika na utii.

Kuutafuta uso wa Mungu siyo tu jambo la kuomba na kuangalia Mungu akijaza maisha yetu na mambo mema. Kuutafuta uso wake inahitaji mabadiliko makubwa. Baadhi ya haya mabadiliko yataumiza. Baadhi yetu tutanyenyekea. Dhambi zitawekwa wazi. Kujitoa kunahitaji kufanyika. Kuutafuta uso wa Mungu ni lazima turudi kutoka njia zetu za uovu.

Cha kuzingatia:

Kuutafuta uso wa Mungu ni jambo rahisi la kuacha Bwana atubariki sisi?Nini kinahitajika kutokea kabla hili kuwezekana?

Nini hutokea wakati Mungu akiangaza uso wake kwetu? Je ni nini uso wake unaonyesha?

Nini kinahitajika kuwa ni kujitoa kwa wale ambao wanautafuta uso wa Bwana?

Kuna muunganiko gani kati ya kutoka katika njia zetu za uovu na kuutafuta uso wa Bwana?

Kwa maombi:

Muombe Bwana afichue vile vitu katika maisha yako unavyohitaji kusema ili kwamba uso wake uangaze kikamilifu zaidi kwako.

Mshukru Bwana kwamba anahitaji kujionyesha yeye mwenyewe kwetu kwa njia ya ndani zaidi.

Muombe Bwana akufanye wewe tayari zaidi kuona dhambi kama anavyoiona.

Muombe Mungu akuongoze wewe katika njia anayotaka wewe kwenda. Omba katika ukamilifu wa baraka zetu kama unvyojiweka katika utiifu.

# 6

# Kisha Nitasikia Kutoka Mbinguni

---

*Kisha nitasikia kutoka mbinguni  (2 Nyakati 7:14)*

Acha tuchukue muda kuzingatia kile tumekiona kufikia hapa kwenye hili somo la 2 Nyakati 7:13-14. Kifungu 13 kinaonyesha tatizo.

*Nikizifunga mbingu isiwe mvua tena nikiamuru nzige kula nchi au nikiwapelekea watu wangu tauni,*

Baraka za Mungu zilikuwa zimezuiliwa sababu ya dhambi, na watu wake hawakupata uwepo wake na kuburudika. Nchi yao ilikuwa imeharibiwa na ukosefu wa mvua, nzige na tauni.

Kama tunavyosogea katika 2 Nyakati 7:14a tunaona utatuzi wa Mungu katika tatizo hili:

*Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu watajinyenyekesha na kuomba na kunitafuta uso na kuziacha njia zao mbaya*

Ikiwa watu wa Mungu wanataka kuona urejesho wa baraka na uponyaji wa nchi yao wanahitaji kujinyenyekeza

wao wenyewe na kuomba. Pia wanahitaji kutafuta uso wa Mungu na kugeuka kutoka njia zao zote za uovu.

Sehemu ya pili ya 2 Nyakati 7:14 inaongea kuhusu mwitikio wa Mungu wakati watu wakifata ufumbuzi wa tatizo lao. Ni muhimu kwamba tunanukuu kwamba ufumbuzi na mwitikio wa Mungu vinahusiana. Sehemu ya kwanza na ya pili ya kifungu cha 14 vinahusiana kwa maneno" ikiwa" na" kisha". Ikiwa watu wa Mungu wakifata ufumbuzi wake kwa tatizo, kisha wangelifahamu majibu mazuri. Uhusiano kati ya maneno" ikiwa" na" kisha" ni muhimu zaidi na hutufundisha sisi somo muhimu sana katika maisha yetu ya kikristo.

Neno" ikiwa" linatoa wajibu kwa watu wa Mungu. Katika swala hili, wakinyenyekeza wao wenyewe, kuomba, na kuutafuta uso wa Mungu na kurudi kutoka njia zao mbaya. Kama tulivyoona, hii inahitaji juhudi kubwa. Neno" kisha" , vyovyote, inatuonyesha sisi kwamba kungelikuwa na zawadi kwa hii juhudi. Baraka za watu wa Mungu, katika swala hili, inategemea katika utayari kufuata ufumbuzi wa Mungu aliopendekeza. Ikiwa watakuwa tayari kumtii Mungu na kukubali ufumbuzi wake, kisha wangelikuwa na uhakika kwamba Mungu angeliwajibu na kuleta upya wake na bulidiko walilolihitaji.

Changamoto tuliyonayo kama waamini ni kuelewa uwiano kati ya neema na wajibu. Kama waamini katika Bwana Yesu Kristo tunaelewa kwamba ukombozi wetu ni jambo la neema. Kwa maneno mengine, hatukustahili kuwa tumesamehewa dhambi zetu. Tusingeliweza kustahiri wokovu Mungu anaoutoa. Ukombozi ni zawadi ya bure kwa wenye dhambi wasio na thamani.

Wote tunafahamu kwamba Bwana huwa anafanya baadhi ya vitu vya ajabu katika maisha yetu. Kama nikitazama kwa namna Bwana akiwa ananibadilisha kwa miaka mingi, nimeuona mkono wake katika yote. Amekuwa akiondoa

mitazamo hasi ndani yangu. Amebadilisha tabia yangu kwa miaka mingi kwa hivyo ninamwitikio kwa njia takatifu zaidi kwa watu na hali mbalimbali. Siwezi kuwa na mashaka na kazi ya Mungu katika maisha yangu na jinsi alivyokuwa neema kuniweka mimi zaidi katika sura ya kristo.

Nina fahamu pia jinsi Mungu anawatumia watu wasio na thamani zaidi kukamilisha kusudi lake. Yona alikimbia mbali kutoka kwa Mungu, bado alitumika kuleta toba kwa mji mzima kule Ninawi. Mwanamke msamalia aliishi maisha ya dhambi lakini alikuwa akitumiwa na Mungu kuwaleta Wasamaria kwa kristo (soma Yohana 4:4-42). Petro alimkanusha Bwana mara tatu lakini alikuwa chombo kilichochaguliwa cha Mungu kuanzisha kanisa lake. Mifano yote hii ni vielezo vya Mungu vya neema ya ajabu. Kila mara hututumia sisi licha ya udhaifu wetu.

Nilikuwa nasema hili, nina tambua pia kuwa kwamba ninawajibu wa moja kwa moja kwa Mungu na kwamba mtazamo wangu au utayari kutii utakuwa na matokeo katika sifa yangu na kuzaa matunda katika huduma. Ninaamini kwamba kuna viwango hatuwezi kuvifikia katika maisha yetu ya kiroho bila kuwa na utii na juhudi. Kuna mfano wa kushangaza wa hili katika Luka 24:13-32. Hapa tuna historia ya Yesu akitembea barabarani kuelekea Emmausi na baadhi ya wanafunzi wake. Hawa wanafunzi hawakumtambua yeye kama walivyokuwa wanamuongelea kuhusu kusulubiwa kwa muda mfupi kwa Bwana wao. Walishirikishana wazi kutokuelewa kwao na Yesu aliwatia moyo kwa maneno ya Mungu. Kitu kisicho cha kawaida kikatokea kwa hawa wanafunzi katika hatima yao. Sikiliza Luka 24:28:

*Wakakikaribia kile kile kijiji walichokuwa wakienda naye alifanya kama anataka kuendelea mbele wakamsihi wakisema” kaa pamoja nasi kwa kuwa kumekuchwa; na mchana unakwisha.” akaingia ndani kukaa nao.*

Nukuu kwamba Bwana Yesu" alifanya kama kwamba alikuwa anaendelea mbele." Hii inatuongoza sisi kuamini kwamba kama isingekuwa kwa juhudi za wanafunzi wake ambo" walibishana kikali" abaki na wao, angeliendelea na kuwaacha warudi nyumbani wao wenyewe.

Matokeo ya mabishano yao makali, vyovyote, ilikuwa kwamba kuja kumuona Kristo yeye ni nani. Ilikuwa ni baada tu walimleta kwenye nyumba yao, kwamba Yesu alionyesha utambulisho wake halisi kwa hao wanafunzi. Maswali yao kuhusu kusulubiwa yalijibiwa wakati walipomtambua yeye kama Bwana Yesu ambaye amekuja katika uzima tena.

Wakati wote mara zote turadhi kwa kidogo katika maisha yetu ya kiroho. Wakati baraka za Mungu zinaangukia hata juu ya pasipo utakatifu (ona Mathayo 5:45) kuna baadhi ya baraka ambazo zinaweza kuwa zetu kupitia uvumilivu na utii shupavu kwa Mungu.

Agano jipya linatufundisha kwamba tutazawadiwa kulingana na uaminifu wetu. Anaongea kupitia mtume Yohana, Bwana Yesu anasema:

*Tazama naja upesi na ujira wamgu u pamoja nami kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo. (Ufunuo 22:12)*

Kitabu cha ufunuo kinatuambia kuhusu taji ambalo wale waliovumilia watalipata kwa uaminifu wao na uvumilivu katika imani (Ona ufunuo 2:10; 3:11). Hii inaashiria kwamba wakati Bwana, katika neema, anaweza hakika kubariki hata wale ambao hawastahili baraka zake, kuna kiwango cha baraka pia ambayo inakuja tu kupitia kufanya kazi kwa bidii na uvumilivu.

Labda kifungu ambacho kinaongea zaidi wazi kuhusu hili ni kinapatikana katika 1 Wakoritho 3:10-15:

*(10) Kwa kadri ya neema ya Mungu niliyopewa mimi kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima naliuweka*

*msingi na mtu mwingine anajenga juu yake lakini mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. (11) Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka isipokuwa na ule uliokwisha kuwekwa yaani Yesu kristo. (12) Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo dhahabu au fedha au mawe ya thamani au miti au majani au manyasi kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri.(13) Maana siku ile itaidhihirisha kwa kuwa yafunuliwa katika moto na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu ni ya namna gani. (14) Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa atapata thawabu. (15) Kazi ya mtu ikiteketea atapata hasara ila yeye mwenyewe ataokolewa lakini ni kama kwa moto.*

Paulo anayafananisha maisha ya kikristo na nyumba inayojengwa. Nukuu kwamba msingi tayari umekwisha umewekwa kwa ajili yetu (1 Wakoritho 3:11). Msingi huo ni neema ya kazi ya Kristo. Nukuu pia kwamba sasa kuna mahitaji ya kujenga kwenye huo msingi. Tunaweza kujenga na aina mbalimbali ya nyenzo. Baadhi ya nyenzo hayatasimama siku ya hukumu. Nyenzo nyingine hazitaweza kustamihili moto na kujaribiwa kwa ubora wa kazi yetu (1Wakoritho 3:12). 1Wakoritho 3:14 inaweka wazi kabisa kwamba ikiwa tutajenga itakayostahimili moto wa hukumu ya Mungu, tutapokea zawadi. Kama sivyo, wakati tukiwa tumeokolewa, itakuwa tu" kama mmoja aliyeepuka kupita katika moto." Kwa maneno mengine, tutakuwa hatuna kitu kuleta kwa Mungu kwa maisha tulioishi katika dunia hii. Tutasimama tukiwa watupu na wenye aibu mbele ya baba yetu wa mbinguni na kutopokea zawadi.

Mwitikio wetu kwa Mungu utatoa matokeo ya umbo na rangi ya maisha yetu ya kiroho. Tunaweza kuwa waaminifu katika kutumia vipawa vyetu vya kiroho na kuona baraka ya Mungu au tunaweza kuzificha hivyo vipawa na kutokuona hizo baraka. Tunaweza kusogea katika wito wa Mungu kwa maisha yetu au tunaweza

kuchagua kutokutii na kutopata kile Mungu anataka kwa maisha yetu. Tunaweza kusimama imara au tunaweza kurudi nyuma. Si kila mara Mungu anaweza kutulazimisha sisi kutii. Wakati akiwa awezi kutuacha sisi, anaweza akaturuhusu tukaenda katika njia zetu wenyewe kwa kipindi cha muda fulani. Kuna waamini ambao wamekufa katika kuasi kinyume cha Mungu. Wengine watachagua njia zao wenyewe na kukataa wito wa Mungu katika maisha yao.

Tunahitaji kufahamu ni kwamba 2 Nyakati 7:14 inatuambia kwamba kuna uchaguzi wa hiari ambao watu wa Mungu wanahitaji kufanya. Maamuzi yao yangelikuwa na matokeo katika umbo la maisha yao. Wangelikataa baraka za Mungu au wangelisalimisha katika ufumbuzi wake na kupata msamaha na uponyaji wake.

Tuna ahadi katika 2 Nyakati 7:14 kutoka kwa Mungu. Hapa anawaambia watu wake kwamba angeliwasikia wao. Ni muhimu kunukuu kwamba tunasikia sauti kwa masikio yetu ya nyama. Mungu hasikii katika njia sawa. Ni kweli kwamba Mungu husikia sauti ya maneno yetu lakini tunakosa jambo muhimu ikiwa tunatafsiri hivyo kifungu hicho. Muktadha unaonyesha kwamba Mungu husikia zaidi kuliko maneno. Husikia mtazamo wetu wakati tukinyenyekeza sisi wenyewe na kuutafuta uso wake kwa moyo wetu wote. Husikia matendo yetu watu tunarudi kutoka njia zetu za uovu. Kusikia kwa Mungu hakuna mipaka kutoa sauti kutoka katika midomo yetu. Anasikia katika njia ambayo hatuwezi kusika. Kwa kweli, baadhi ya maombi ya nguvu hayatengenezwi hata kwa maneno. Mara nyingine maneno hayajitoshelezi kuelezea ukamilifu wa kile kilicho katika moyo. Mungu husikia huko kuvunjika kwa moyo wetu. Husikia matendo yetu ya toba. Husikia hamu ya mioyo yetu ambayo haiwezi kuelezeka katika maneno. Mungu havutiwi na maneno tu. Huvutiwa katika mitazamo na matendo. Hiki ndicho Mungu anasema

atasikia, na wakati anasikia mioyo iliyovunjika ikipiga kelele katika unyenyekevu na matendo, alituhaidi kujibu.

Hakuna tena undani zaidi tunaohitaji kuuona katika sehemu ya kifungu hiki cha 14. Nukuu kwamba Bwana anasema kwamba angelisika kutoka mbinguni. Hii ni muhimu. Kuna njia tatu tungelielewa hili. Kwanza, Mungu husikia kutoka mbinguni ni kwamba hapa ni pale anakaa. Wakati hii ni, katika sehemu, kifungu kinasema nini, kuna hisia za ndani katika kifungu" kutoka mbinguni."

Njia ya mbinguni haiwezi kupewa changamoto. Wakati kifungu kinatuambia kwamba Mungu husikia kutoka mbinguni, hutupa utawala mkubwa katika ahadi hii ya Mungu. Maombi yetu ya maneno, mtazamo na matendo yamemfikia Mungu mbinguni. Ni sasa katika mikono ya mmoja ambaye anayo mamlaka kamili. Amesikia maombi yetu na amehaidi kuchukua hatua kutoka katika kiti chake cha mamlaka. Hakuna kitu kinaweza kusimama katika njia yake. Hakuna jambo lisilowezekana kwake. Asili lazima imsikilize. Maadui lazima wanyamaze. Miujiza inaweza kutokea kwa sababu Mungu mwenye mamlaka na nguvu sasa amesimama kutoka kwenye mamlaka yake mbinguni na kuja kutusaidia sisi.

Kifungu" kutoka mbinguni" siyo tu inatupa mamlaka katika mahitaji yetu lakini pia inatuambia sisi kuhusu asili ya baraka ambayo ni matokeo ya maombi yetu. Maombi yamesikiwa mbinguni. Hii inamaanisha kwamba mwitikio kwa mahitaji yetu yatakuja kutoka mbinguni. Majibu kwa mahitaji yetu ni majibu ya kimbingu na siyo ya kidunia tu. Hii inamaanisha kwamba inaweza kuonekana tofauti kabisa kutoka kile tunachokitegemea. Sikiliza kwa kile Bwana alichosema kupitia Isaya katika Isaya 55:8-9:

*(8) Maana mawazo yangu si mawazo yenu wala njia zenu si njia zangu asema Bwana. (9) Kwa maana kama*

*vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu na mawazo yenu.*

Baraka za mbinguni zina vipaumbele mbalimbali. Tamanio la Mungu ni kwa ustawi wa kiroho chetu na urafiki wake kwetu. Wakati mwingine hizi baraka zinaweza kutokea kwetu kama jaribu. Kifo cha Bwana Yesu juu ya msalaba hakikuonekana kuwa baraka kwa wakati huo, lakini mbegu iliyopandwa siku hiyo ilifanyika msingi wa kazi ya ufalme wa Mungu katika vizazi vyote. Ahadi Mungu alizoahidi zinatoka mbinguni. Ni kweli kwamba vitu vya kushangaza vinaweza kutokea juu ya dunia hii kama matokeo ya baraka zambinguni, lakini tusingeliziwekea mipaka baraka hizi kwa mali za mwili, faraja na urahisi. Kufanya kwa kupunguza baraka nyingi kubwa ambazo Mungu anataka kutupa.

Katika Isaya 64:1-4 Nabii anamuita Mungu kufungua mbingu na kuja chini. Katika uhalisia anamuita Mungu kumimina baraka zake za mbinguni juu ya dunia. Sikiliza katika maombi haya:

*(64:1) Laiti ungepasua mbingu na kushuka ili milima itetemeke mbele zako. (64:2) Kama vile moto uchomapo vichaka na moto uchemshapo maji ili kuwajulisha adui zako jina lako mataifa wakatetemeka mbele zako!(64:3) Ulipofanya mambo ya kutisha tusiyoyatazamia ulishuka milima ikatetemeka mbele zako. (64:4) Maana tangu zamani za kale watu hawakusikia wala kufahamu kwa masikio wala jicho halikuona Mungu ila wewe atendaye mambo kwa ajili yake amngojaye.*

Zingatia asili ya baraka za Isaya alizokuwa anaita chini kutoka mbinguni katika Isaya 64. Baraka hizi zingesababisha milima kutetemekaa Isaya 64. Inaelezewa kama moto uchomapo vichaka au kusababisha maji kuchemka. Ilikuwa ni kama tetemeko kubwa la aridhi ambalo linasababisha taifa la adui kutetemeka. Hii ni aina

ya baraka ungeliomba siku ya leo? Baraka hizi zinanguvu kubwa ya matokeo ya utakaso juu ya dunia. Wenye dhambi watatetemeka na kuogopa gadhabu ya Mungu. Waamini hushuka magotini wakinyenyekea na kuvunjika. Mungu anatembea katika njia tusiyoweza kuelezea. Ufalme wake ulianzishwa na dhambi na uasi ni viti vilivyo shindwa kwa nguvu. Tunaweza kufikiri tu matokeo ya aina hii ya baraka tungelikuwa nazo katika makanisa yetu leo. Wanafiki wangelikuwa wamewekwa wazi na kuondolewa. Watu wa Mungu wangelikuwa wanyenyekevu na wamepewa vifaa kwa huduma kubwa. Mahusiano yangelituzwa. Baraka za Mungu wa mbinguni siyo tu kuhusu maisha ya kustarehe zaidi. Ikiwa kitu chochote, tunaweza kutafuta faraja ya changamoto. Tunaweza kujikuta sisi wenyewe tumejihusisha katika vita inayohusisha kujitoa sana. Tunaweza kulazimika kutoa vyote tulivyonavyo. Wakati baraka za mbinguni zinamiminwa araka za kidunia zinajisalimisha.

Kwa kuzingatia:

Tunajifunza nini kuhusu hali ya asili ya baraka za Mungu katika kingu hiki? Kuna baraka zozote tutakazo pokea tu ikiwa tumekutana na mahitaji fulani?

Umekuwa ukikosa baadhi ya baraka za Mungu anazotamani kukupa? Kwa nini?

Kuna tofauti gani kati ya baraka tunazo pokea kama matokeo ya ajabu ya neema ya Mungu na baraka tunazo pokea kama zawadi kwa huduma ya uaminifu na utiifu?

Namna gani pamoja ya haya yanaweza kuonekana kama tendo la neema katika sehemu ya Mungu?

Kuna tofauti gani kati ya baraka za mbinguni na baraka za duniani? Tumekuwa na hatia ya kutafuta baraka za duniani tu?

Ni kanisa la siku zetu lipotayari kupokea baraka kutoka mbinguni? Unafikria nini hizi baraka zingelionekana kuwa? Ni matokeo gani yangelikuwa juu ya waamini?

Kwa maombi:

Mshukru Bwana kwamba ni Mungu wa neema ambaye anatubariki sisi hata wakati hatustahili hizo baraka.

Mshukru Bwana kwamba kuna baraka katika stoo kwa wale ambao wanatembea katika utiifu na kujisalimisha kwake. Muombe akupe neema ya kutembea katika utiifu ili kwamba uweze kupata baraka hizi pia.

Muombe Bwana kuandaa watu kwa baraka anayotaka kuimimina juu yao. Muombe yeye atutoe kutoka kupenda dunia hii ili kwamba tuweze kupata baraka kubwa za mbinguni anazotaka kutupa sisi.

# 7

# MSAMAHA NA UPONYAJI

*…na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao (2 Nyakati 7:14)*

Tumekuwa tukichunguza mwitikio wa Mungu katika maombi ya Sulemani katika 2 Nyakati 6. Ombi la Sulemani lilikuwa kwamba wakati watu wa Mungu wanaanguka katika dhambi, Mungu angelisikia maombi yao, kusamehe dhambi zao na kuwarejesha wao kwenye ushirika na baraka (Ona 2 Nyakati 6:21, 23, 25, 27, 30, 39). Mungu alikuwa tayari kufanya hili, lakini alihitaji kwamba watu wake kwanza wajinyenyekeze wao wenyewe, kuomba, kuutafuta uso wake na kurudi kutoka kwenye njia zao za uovu. Katika sura hii ya mwisho tutaangalia katika ahadi ya Mungu wakati hii hali ilipofikiwa.

## MUSAMAHA

Ahadi ya Mungu kufanya mambo mawili katika sehemu ya mwisho ya kifungu cha 14. Ya kwanza ya ahadi hizi mbili ilikuwa ni msamaha. Hili lilikuwa ni hitaji kubwa la watu wa Mungu. Walitenda dhambi dhidi ya Mungu mtakatifu na

walikuwa chini ya hukumu yake. Dhambi yao iliwatenga wao siyo tu kutoka katika ushirika na Mungu lakini pia kutoka katika baraka zake. Wakati tu uhusiano wao uliporejeshwa wangelikuwa mara moja tena wamepata urafiki na Mungu wao na ukamilifu wa kusudi lake.

Nukuu katika kifungu hiki uhusiano kati ya msamaha na uponyaji wa nchi. Nchi ilkuwa inahangaika kwa sababu watu wa Mungu wamegeuka kutoka kwake. Hii inatuonyesha sisi kwamba dhambi inaweza kuwa na madhara katika nchi yetu. Wakati watu wa Mungu hawapo sawa na yeye, hii itakuwa ni ushahidi katika hali ya jamii yetu. Wakati Wakristo wakiwa hawako sawa wanavyopaswa kuwa, jamii yao itakuwa imetumbukia katika giza.

Nukuu pia katika kifungu hiki kwamba ni waamini wanaohitaji msamaha huu. Sifa hizi baadhi za kuzingatia. Kuna wale ambao wanaamini kwamba kwa sababu ya Bwana Yesu alikufa juu ya msalaba atusamehe dhambi zetu, waamini hawahitaji kuomba msamaha. Inawezekana kwa muamini kuwa na kutokusamewa dhambi katika maisha yake sasa, tangu Yesu amekufa na kulipia dhambi zetu, jana, sasa na kesho?  Waamini watasimama mbele za Mungu na kutoa hesabu ya dhambi katika maisha yao?

Kuna ushahidi uliowazi katika maandiko kwamba ingawa Bwana Yesu alilipa kwa dhambi juu ya msalaba bado tunahitajika kuja kwake kusamehewa. Waumini wengi watapata aibu kama watakavyo simama mbele za Mungu katika siku hiyo ya mwisho. Yesu aliiweka wazi katika Mathayo 12:36 kwamba tutatakiwa kutoa hesabu katika kila" neno lisilo na maana"  tuliloliongea:

Basi nawaaambia kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu watatoa hesabu ya neon hilo siku ya hukumu.

Katika Mathayo 6 Bwana Yesu alikuwa anawafundisha wanafunzi wake namna ya kuomba. Moja ya mahitaji

katika maombi ya Bwana ni kwamba Mungu angewasamehe wao makosa yao kama tunavyowasemehe wengine. Yesu aliendа kusema ikiwa hatuwasamehi wengine wakati wakitenda dhambi dhidi yetu kisha baba wa mbinguni hatatusamehe sisi.

*(14) Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao na baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. (15) Bali msipowasamehe watu makosa yao na baba yenu wa mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.*

Kumbuka kwamba Bwana Yesu anaongea kwa wanafunzi wake wakati anatengeneza hiki kipengele. Hii inatuonyesha wazi kwamba inawezekana kabisa kwa muamini kuwa hajasamehewa dhambi katika maisha yake.

Inaandikwa katika 1Yohana 1:8-10, mtume anaweka wazi kabisa kwamba hata waamini bado dhambi iko ndani yetu ambayo inahitaji kuwa imesamehewa.

*(8) Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenyewe wala kweli haimo mwetu. (9) ukiziungama dhambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote. (10) Tukisema kwamba hatukutenda dhambi twamfanya yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu.*

Ikiwa Yesu alikuja kusamehe dhambi na kutuleta kwenye uhusiano na baba, inawezekanaje kuwa na kutosamehewa dhambi katika maisha yetu? Kuna kifungu kizuri katika Yohana 13 ambayo ni msaada sana katika kuangalia huku. Katika Yohana 13 Bwana Yesu alikuwa anakula pasaka yake ya mwisho na wanafunzi. Wakati wa chakula cha jioni, Bwana Yesu alitoka kwenye chakula na, akachukua taulo, aliendelea kuwaosha wanafunzi miguu. Petro alikuwa na tatizo hasa Yesu kuosha miguu yake.” Hautaosha kamwe miguu yangu,” alimwambia Yesu siku

hiyo (Yohana 13:8). Yesu alimuelezea kwamba isipokuwa kumuosha Petro, asingelikuwa na nafasi ya kwake. Petro aliposikia hivyo, alikubali:

*Simoni Petro," akamwambia Bwana" "si miguu yangu tu hata na mikono yangu na kichwa change pia!" (Yohana 13:9)*

Petro alitaka Bwana kumuosha kutoka kichwani hadi kidole cha miguu. Yesu akamjibu Petro siku hiyo ni muhimu:

*Yesu akamwambia yeye aliyekwisha kuoga hana haja ya ila ya kutawadha miguu bali yu safi mwili wote nanyi mmekuwa safi lakini si nyote.*

Yesu alikuwa anamuambia Petro nini hapa? Alimwambia yeye kwamba mtu ambaye amekwisha kuoga ni safi na anahitaji tu kuosha miguu. Fikiria umeishi Yerusalemu katika siku hizo za Yesu. Rafiki zako wanakualika kwa chakula cha jioni. Katika maadalizi ya hicho chakula, unaoga. Unavaa nguo zako nzuri unatoka nje ya mlango na kutembea kwenye barabara za vumbi za Yerusalemu kuelekea kwenye nyumba ya rafiki yako. Unafika mlangoni unagundua kwamba vumbi la barabarani limekuchafua miguu yako. Baada ya kuwasili unasalimiwa na mtumishi akiwa na beseni la maji. Unavyokaa, mtushi huyu anapiga magoti na kukuosha mavumbi ya miguu yako na mara moja tena unakuwa safi kabisa. Hauitaji kuoga kwa ajili ya miguu yako michafu. Yote unayohitaji kufanya ni kuosha mavumbi na kuwa safi tena.

Yohana 13 ina mambo baadhi muhimu ya kutufundisha kama waamini. Bwana Yesu ametusafisha kwa kifo chake juu ya msalaba. Kwa sababu tu safi tunaweza kuja kwa baba, kusafishwa dhambi na uchafu wetu. Dhambi haitatutenganisha tena sisi na Mungu kwa sababu ya kazi ya Bwana Yesu juu ya msalaba. Tumeoshwa ndani ya

damu yake na kusafishwa doa la dhambi katika maisha yetu.

Wakati tunasafishwa kwa damu ya Bwana Yesu, bado tunatembea kwenye vumbi na uchafu wa mtaani wa dunia hii ya dhambi. Kama tunavyotembea katika hii dunia, tunaathiriwa na uchafu wake. Macho yetu yanaona vitu vinayotusabisha sisi kutenda dhambi. Masikio yetu yanasikia vitu ambavyo vinatupa hasira na kusababisha kuitia katika hali isiyokuwa ya utakatifu. Ndimi zetu zinaongea mambo ambayo yanaumiza kaka na dada zetu. Nani miongoni mwetu hajapewa katika asili msukumo wa mwili? Kama tunavyoishi katika ulimwengu huu, tunajikuta sisi wenyewe tumejaribiwa kufanya dhambi. Kama ilivyo hakuna mtu angelitembea katika vumbi la mtaa wa Yerusalemu bila miguu yake kuchafuka, hivyo hakuna mmoja wetu atakuwa anaweza kuishi katika ulimwengu huu bila kuwa amechafuliwa na dhambi na majaribu yake.

Wakati tulipooga na kusafishwa katika damu ya kristo, bado tutahitajika kuja kila mara kwa Bwana kwa" kuoshwa miguu kiroho" tutatakiwa kukiri kushindwa kwetu. Tutahitaji kila siku kusafishwa kwa Bwana wetu. Bwana amehaidi kusamehe na kutuosha dhambi ya kila siku. Wakati hizi dhambi hazisababishi kupoteza ukombozi wetu, zitaathiri uhusiano wetu na baraka. Ikiwa tunataka kufahamu upya wa huo ushirika na baraka, tutahitaji kuja kila mara kwa Bwana kwa msamaha na kusamehewa.

## UPONYAJI

Kitu cha pili Mungu amehaidi kufanya kwa watu wake katika sehemu ya mwisho ya kifungu cha 14 ilikuwa ni kuponya nchi yao. Dhambi inaleta ugonjwa na kifo. Ufumbuzi kwa hili ni kusamehe. Msamaha unaondoa vikwazo vya uzima na kifo.

Hiki ni kitu tusichoelewa kila mara kama waamini. Wakati tunaona hivyo makanisa yetu hayana afya, tunajaribu kurekebisha kwa kuongeza shughuli fulani au kubadili shughuli zetu za sasa. Wakati hili linaweza kuwa muhimu, siyo kila mara ni msingi unaohitajika. Kubadilisha mpango hautabadili moyo. Inaweza kuwafanya watu wenye furaha kwa muda lakini haiwezi kubadili sababu ya msingi ya kukosa baraka za Mungu.

Ninaamini kwamba Maungu anahitaji sisi tupate baraka zake kamilifu zaidi kuliko tunavyohitaji kuzipata. Ni furaha yake kumtuma mwanae ili kwamba tufanyike watoto wake. Ni tamanio lake kutumwagia zawadi nzuri. Yesu aliliweka wazi hili katika Mathayo 7:11 wakati anasema:

*Basi, ikiwa ninyi mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! si zaidi sana baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?*

Furaha ya baba ni kuwabariki watoto wake. Huhuzunika wakati watoto wake wasipotembea katika ukamilifu wa baraka zake. Mtume Paulo anatukumbusha sisi katika 1Wakoritho 2:9:

*Lakini, kama ilivyoandikwa: “mambo ambayo jicho halikuyaona wala siko halikuyasikia (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.”*

Hatujaona chochote kama baraka Mungu alizonazo kwa ajili yetu. Masikio yetu hayajawahi kusikia aina ya ukamilifu wa ajabu na furaha. Hata kwenye mawazo yetu ya ndani, tusingeliweza kupata ukubwa na utajiri wa Mungu alionao kwenye ghala kwa wale ambao wanampenda yeye. Huo ni moyo wa Mungu kwa watoto wake. Ni nini hicho kinacho tutenga na baraka hizi? 2 Nyakati 7:13-14 inatuambia sisi kwamba hiyo ni dhambi. Ikiwa baraka hizi zinatakiwa kurejeshwa ni lazima tuondoe vikwazo. Ili nchi yetu iwe na

afya tena, itachukua nafasi tu kupitia msamaha wa dhambi.

Wakati mwingine huenda kujikuta katika vita ya kiroho na adui. Ninafahamu kwamba Bwana Mungu ameniita mimi kwenye huduma ya kuandika na kufundisha ulimwengu wake. Natumia asubuhi kufanya kazi kwenye vifungu vya maandiko na kurudi nyumbani kutoka duka la kahawa ambapo nilikuwa nafanya kazi. Nikiwa natembea kwenda nyumbani, ninamsikia adui anazungumza kwenye akili yangu akisema:" unafikri nini unafanya? Kipi chema kuandika fafanuzi hizi za biblia? " Wakati nilipofahamu hii inatoka kwa shetani, maneno hayo yalikaa akilini kwangu kwa siku nzima nilisumbuliwa na maneno hayo.

Siku iliyofuata, Wakati ninarudi kuelekea duka la kahawa tena kuandika, Bwana akaongea na mimi kwa nguvu sana kwamba vunja athari ya maneno hayo kutoka kwa shetani. Alinikumbusha mimi kwamba kulikuwa na matatizo katika jamii yetu kwamba sayansi, siasa au dawa zisingeliweza kurekebisha. Matatizo haya yangeliweza kutatuliwa tu kwa neno la Mungu. Mungu alinikumbusha mimi kwamba ikiwa jamii yetu ingelitembea katika neno lake wangelibadilishwa.

Fikri nini kingelitokea katika taifa letu ikiwa wangerikili dhambi zao na kujitoa kwao wenyewe kumtafuta Mungu na kutembea kulingana na kanuni zake? Hii dunia ingelikuwaje ikiwa watu wangetambua kwamba wametenda dhambi na kukiri hiyo dhambi wakajitoa wao wenyewe kumtafuta Mungu peke yake? Kanisa lako lingekuwaje ikiwa huu ni mtazamo? Serikali zetu zingelibadilika. Mahitaji yangelikamilika. Uchumi wetu ungelibadilika. Mataifa yangelisitisha vita. Ugonjwa wa nchi yetu ungeliponywa na baraka za Mungu zingelinyesha kwetu.

Hatimaye, matatizo katika nchi yetu yanafanywa pamoja na dhambi. Uchoyo, kujisifu, ubinafsi, tamaa na dhambi nyingine zimesababisha nchi hii ya kwetu kuugua magonjwa. Hii ni kweli siyo tu katika nchi yetu lakini pia katika makanisa yetu na maisha binafsi. Hitaji kubwa la siku zetu ni uponyaji wa makanisa na nchi yetu. Kizuizi kikubwa kwa hili ni dhambi. Ufumbuzi ni kunyenyekea sisi wenyewe na kuomba, kuutafuta uso wa Mungu na kurudi kutoka njia zetu za uovu. Kisha tu Mungu atasikia kutoka mbinguni, asamehe dhambi zetu na kuponya nchi yetu. Mungu atupe neema kujifunza somo la kifungu hiki rahisi cha maandiko ili kwamba mara moja tena tupate ukamilifu wa baraka zake katika maisha yetu, kanisa na mataifa.

Cha kuzingatia:

Je Wakristo wanahitaji kusamehewa? Namna gani dhambi inaathiri ushirika wetu na Mungu na ukamilifu wa maisha yake ndani yetu?

Kuna mtu yeyote amekutenda dhambi wewe unahitaji kushughulikia katika maisha yako leo? Ni kina nani hao? Ni madhara gani ya dhambi hii ipo unayo wewe?

Ni baadhi ya njia gani tumechagua kufanyia kazi kwa ukosefu wa baraka na magonjwa katika makanisa yetu na nchi? Namna gani shetani anatafuta kutuweka sisi kutoka kufahamu uhusiano kati ya dhambi na kukosekana kwa baraka?

Kwa maombi?

Muombe Bwana akupe neema ya kuwa tayari kujichunguza wewe mwenyewe katika mwanga wa ulimwengu wake. Muombe aonyeshe dhambi yoyote katika maisha yako ambayo ingelikuweka kutoka katika ukamilifu wake.

Mshukru Bwana kwamba alikufa ili kwamba adhabu kwa dhambi zetu zote zilikuwa zimelipwa.

Mshukru Bwana kwamba wakati tunakuja kwake kwa ajili ya kusafishwa kila siku, anaongeza musamaha wake kwetu.

Muombe Mungu atembee katika maisha yako na katika jamii yako kuleta roho ya kukiri na toba.

Mshukru Bwana kwamba tamanio lake kubwa ni kubariki watoto wake. Muombe yeye atembee kwa nguvu kati yetu kama watoto wake ili kwamba vikwazo vya dhambi viondolewe.

# Light To My Path Book Distribution

Light To My Path (LTMP) ni huduma ya uandishi na usambazaji iliyowafikia kwa wafanyakazi wahitaji Wakristo katika Asia, America kusini, na Afrika. Wafanya kazi Wakristo wengi kwenye nchi zinazoendelea hawana rasilimali muhimu za kupata mafundisho ya biblia au kununua vifaa masomo ya biblia kwa huduma zao na kutiwa moyo kwa mtu binafsi. F. Wayne Mac Leod ni mwanachama wa Action International Ministries na amekuwa akiandika vitabu hivi kwa lengo la kuvisambaza kwa wa Wachungaji wahitaji na Wakristo wafanya kazi duniani kote.

Adi sasa makumi elfu ya vitabu yamekuwa yakitumika kwenye, mahubiri, mafundisho, uinjilisiti na faraja kwa waumini wa ndani kwenye zaidi ya nchi sitini. Vitabu vimekuwa sasa vikitafsiriwa kwa lugha nyingi. Lengo ni kuvifanya viwe vinapatikana kwa waumini wengi kama inavyowezekana.

Huduma ya LTMP ni huduma ilijikita kiimani na tunaamini Bwana kwa rasilimali muhimu kwa kusambaza vitabu kwa kufariji na kuimarisha waaminini duniani kote. Wewe

utaomba kwamba Bwana ange lifungua milango kwa kutafsiri na kusambazwa zaidi kwa vitabu hivi?

Kwa habari zaidi kuhusu Light To My Path Book Distribution tembelea mtandao wetu kwenye www.lighttomypath.ca